



# UMOJA - ONE UN in Tanzania

## UNIDO kuendeleza ushirikiano na Serikali kuhusu uchumi wa viwanda

Toleo la. 77  
March - April 2018



Mkurugenzi Mkuu wa UNIDO, LI Yong (kulia) na Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mh. Samia Suluhu Hassan (kushoto). Nyuma yao (kutoka kushoto kwenda kulia) ni Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji, Mh. Charles Mwijage na Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Dkt. Augustine Mahiga. **Picha | Ikuu**

Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la lengo la kuimarisha ushirikiano na Umoja wa Mataifa la Maendeleo ushirika wa kimkakati na nchi hii. ya Viwanda (UNIDO), LI Yong, hivi karibuni alitembelea Tanzania kwa Wakati wa ziara yake, LI Yong

### Vidokezo

- **Siku ya Kimataifa ya Wanawake**
- **Vijana wa Kigoma waonja manufaa ya Msaada wa UN**
- **UN & Wahariri watia saini makubaliano ya kanuni za ushirikiano**

alikutana na Makamu wa Rais, Mh. Samia Suluhu Hassan, na mawaziri kadhaa. Walifanya mazungumzo mapana kuhusu vipaumbele vya Serikali katika maendeleo ya viwanda na suluhu endelevu ambazo UNIDO inaweza kusaidia, hasa katika juhudi zinazoendelea nchini. Baadhi ya masuala yaliyojadiliwa, mionganini mwa mengine, ni umuhimu wa kuimarisha ushirika na pande mbalimbali ili kuleta ujumuishi na maendeleo endelevu yaviwanda, nanafasiya ushirikiano wa viwanda kwa Mataifa ya Kusini-Kusini katika kuimarisha teknolojia na uhamishaji ujuzi. Wakati wa ziara hiyo, tamko la **Inaendelea Ukurasa wa 2**

### Kauli ya Serikali:

**"Ningependa kupongeza juhudi za viongozi vijana na wanaojitolea kutoka katika Chama cha Vijana wa Umoja wa Mataifa cha Tanzania kwa kuuleta pamoja mjumuiko huu wa vijana motomoto kutoka Tanzania nan je ... Tunaamini kwamba mawazo yenu yatachangia katika juhudi za 'kutekeleza ajenda ya 2030'. Tungependa kutambua msaada uliotolewa na waungaji mkono wote; hasa, Umoja wa Mataifa."**

**Mh. Anthony Mavunde, Naibu Waziri wa Nchi katika Ofisi ya Waziri Mkuu mwenye dhamana ya Sera, Masuala ya Bunge, Kazi, Ajira, Vijana na Walemau mnamo Aprili 30, 2018 jijini Dodoma kwa niaba ya Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mh. Samia Suluhu Hassan.**

### **kutoka ukurasa wa 1**


pamoja la kuimarisha ushirikiano kati ya UNIDO na Serikali ya Tanzania lilitiwa saini ili kuunga mkono utekelezaji wa Dira ya Maendeleo ya Taifa ya 2025; Dira ya Zanzibar ya 2020; Mpango Endelevu wa Maendeleo ya Viwanda, na Mkakati Uganishi wa Tanzania wa Maendeleo ya Viwanda wa 2025 (IIDS 2025). Mikutano mingine iliyofanyika ilijumuisha ile ya pamoja na wawakilishiwasektabinafsi, vyama vya kiraia na Timu ya Menejimenti ya Nchi ya Umoja wa Mataifa.

Baada ya mikutano katika jiji la Dar es Salaam, Mkurugenzi Mkuu LI alielekea Zanzibar ambako alikutana na Rais Dkt. Ali Mohamed Shein na Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko, Mh. Amina Ali, kujadiliana umuhimu wa kuimarisha ushirikiano kwa lengo la kusukuma maendeleo ya viwanda yaliyo jumuishi na endelevu huko Zanzibar.

Kama sehemu ya uungaji mkono

unaofanywa na UNIDO katika kilimo cha mwani huko Zanzibar, ambapo zaidi ya asilimia 90 ya wakulima na wanachama

wa vyama vya wachakataji ni wanawake Shirika lilitoa takribani Shilingi milioni 180 (Dola za Marekani 80,000).



Mkurugenzi Mkuu wa UNIDO, LI Yong (kushoto) alikutana na Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, H.E. Ali Mohamed Shein (kulia), Wakati wa ziara yake Tanzania. **Picha | Ikulu / Zanzibar**

## **IOM yawarejesha wahamiaji sita wa Ethiopia waliokuwa wamefungwa, wengine 913 wangali katika magereza ya Tanzania**



Wasichana sita raia wa Ethiopia waliokuwa wamefungwa katika magereza nchini Tanzania wakiwasili kiwanja cha ndege tayari kurejeshwa kwao. Shirika la IOM liliwasafirisha kwa usalama raia hao wa Ethiopia. **Picha | IOM Tanzania**

Mnamo mwezi Machi, Shirika la Umoja wa Mataifa la Wahamiaji (IOM) nchini Tanzania liliendesha mpango wa kubaini utaifa kwa wahamiaji wasio rasmi waliodaiwa kutoka Ethiopia waliokuwa wametiwa nguvuni katika magereza sita ya Tanzania, yaani, magereza ya Bukoba, Kitengule Prison, Butimba, Maweni, Kigongoni na Gereza la Keko.

Lengo kuu la mpango huo lilikuwa kuthibitisha utambulisho wa wahamiaji ili kuwasidia warejee makwao chini ya utaratibu wa Msaada wa Urejeshwaji Nyum-

bani kwa Hiyari, yaani, Assisted Voluntary Return and Reintegration (AVRR). Mpango huo ulifanikiwa kuwatambua na kuwathibitisha raia 919 wa Ethiopia—miongoni mwao sita wakiwa wanawake.

Wahamiaji 300 walichaguliwa ili kuperwa msaada huo wa kibinadamu wa kurejeshwa makwao mara moja kwa kuanzia na raia wale sita wa Ethiopia wanawake ambaeo tayari wamerejeshwa nchini kwao.

Wahamiaji 294 wengine watasaidiwa kurejea kwao mwezi Mei, 2018.

IOM inaendelea na jitihada za kufatuta rasilimali zaidi ili kuwezesha usafirishwaji wa wahamiaji wengine 619 waliotambuliwa na ambaeo bado wako katika magereza huko Mwanza, Dar es Salaam, Kagera, Tanga na Mkoa wa Pwani.

# UN na Wahariri kushirikiana katika kuandika habari za Malengo ya Dunia



Kaimu Mwenyekiti wa Jukwaa la Wahariri Tanzania, Bw. Deodatus Balile (kushoto) na Mtaalamu wa Mawasiliano wa UN, Bi. Hoyce Temu (kulia) wakibadilishana hati za makubaliano ya kanuni za ushirikiano. Picha | Edgar Kiliba UNRCO

Umoja wa Mataifa Tanzania (UN Tanzania) na Jukwaa la Wahariri Tanzania (TEF) zimetiliana saini makubaliano kuhusu kanuni za ushirikiano ambazo kwazo zitaimarisha mawasiliano na utetezi kwa ajili ya utekelezaji wa Malengo ya Dunia nchini Tanzania.

Ushirikiano kati ya TEF na UN umedumu kwa zaidi ya miaka 5 sasa ambapo wakuu wa mashirika ya UN hukutana na waandishi wa habari na wahariri waandamizi mara moja kwa mwaka. Ushirikiano wa hivi karibuni unaendeleza ushirika kwa lengo la kuandika habari za maendeleo katika muktadha wa utekelezaji wa Malengo ya Dunia kupitia Mpango wa Pili wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano na Mpango wa Pili wa Msaada wa Maendeleo wa Umoja wa Mataifa (UNDAP II).

Kupitia makubaliano hayo, UN na TEF kwa pamoja zitajenga uwezo wa waandishi kutoka katika mikoa ilio kwenye kanda tano za Tanzania

ili kuhakikisha kwamba utekelezaji wa Malengo ya Dunia unaripotiwa katika ngazi ya mahalia. Hii itajamuisha ziara katika miradi muhimu ya UN na Serikali ili kuangazia njia bora zinazotumika na changamoto zilizopo katika utekelezaji wa Malengo ya Dunia. Ushirikiano huo pia utaanlisha tuzo ya Umahiri wa Uandishi wa habari kwa waandishi watakoafanya vizuri katika kuandika habari za Malengo ya Dunia na kazi za Umoja wa Mataifa nchini Tanzania.

Akizungumza kwa niaba ya Mratibu Mkazi wa UN katika Mkutano wa TEF, Mtaalamu wa Mawasiliano wa UN, Bi. Hoyce Temu, aliangazia umuhimu wa kushirikiana kwa karibu kati ya vyombo vya habari ili kuuelimisha umma kuhusu Malengo ya Dunia. "Tunathamini kazi inayofanywa na vyombo vya habari katika kutambua kwamba wao ni wadau muhimu katika kutoa taarifa juu ya mafanikio katika utekelezaji wa Malengo ya Dunia," alisema Bi.

Temu.

"Jukumu lenu kama wahariri ni kuangazia masuala yanayoikabili nchi ni makubwa na yanastahili pongezi. Tunapoendelea kushirikiana na Serikali kuboresha maisha ya jamii, tunatazamia kuimarisha ushirika wetu na wadau wa vyombo vya habari kote nchini."

Kwa upande wake, Kaimu Mwenyekiti wa TEF, Bw. Deodatus Balile, alisema makubaliano yataimarisha ushirika kati ya TEF na UN na kwamba mafunzo kwa waandishi wa habari yatatoa mchango mkubwa katika mikoa hiyo.

*"Tunathamini kazi inayofanywa na vyombo vya habari katika kutambua kwamba wao ni wadau muhimu katika kutoa taarifa juu ya mafanikio katika utekelezaji wa Malengo ya Dunia,"*  
**Bi. Hoyce Temu**

## Vijana wa Kigoma wanufaika na Msaada wa awali wa UN

Mwezi Aprili, Mkuu wa Wilaya ya Kigoma, Bw. Samson Anga; Mratibu Mkazi wa UN Tanzania, Bw. Alvaro Rodriguez; na Kikosi Kazi cha Mawasiliano cha UN (UNCG), maofisa kutoka mashirika 15 ya UN Tanzania; na vyombo vya habari walitembelea vijana na wanawake walionufaika na programu za pamoja za UN katika Mji wa Kigoma.

Programu ya Pamoja ya Kigoma (KJP) inaongezea katika jithada za kibinadamu za mkoani Kigoma na inaendeleza hatua zilizochukuliwa hapo kabla na UN kama vile mradi wa pamoja wa Kigoma wa UN uliofadhiliwa na ILO, UNIDO, UN Women na FAO katika eneo la uvezeshaji vijana. Programu hii ya pamoja iliendeshwa kwa ushirikiano na AZISE ya mkoani humo ya Nyaktonto Youth for Development Tanzania pamoja na Manispaa ya Kigoma. Zaidi ya vijana 110 walipata mafunzo kuhusu uanzishaji na uendeshaji biashara. Vijana waliopata mafunzo hivi sasa wanaendesha shughuli zao kama vile kilimo, kilimo cha mbogamboga na matunda na uten-genezaji sabuni.

Ziara za uwandani zilifanyika katika eneo la uzalishaji la vijana waliope-wa mafunzo na Kituo cha Vijana cha Nyaktonto. Vijana hao waliopata mafunzo chini ya programu hii walonyesha baadhi ya shughuli zao za ujasiriamali kama vile uchakataji



Mmoja wa watu walionufaika na programu ya pamoja ya awali ya UN katika Mji wa Kigoma akiwaonyesha wajumbe namna ya kukamua mafuta kutoka kwenye biwi la miwese. Photo| Msafiri Manongi/KJP

sabuni. Mkuu wa Wilaya, Bw. Samson Anga, aliwapongeza vijana kwa mafanikio yao na aliishukuru UN kwa kushirikiana na Serikali katika juhudzi za kunyanya maisha ya vijana. "Tumeona jinsi vijana hawa wanavyotengeneza sabuni. Na, tumeona pia changamoto wanazokabiliana nazo—kuna haja ya sisi kuongeza msaada zaidi kwao," alisema.

Akizungumza wakati wa ziara hiyo ya uwandani, Mratibu Mkazi wa UN, Bw. Alvaro Rodriguez, alisema kwamba, "Matokeo ya programu ya

awali ya pamoja kati ya mashirika ya UN kwa kushirikiana na maonyesho ya Nyaktonto, tunaweza kuleta matokeo mazuri kwa kufanya kazi pamoja kwa karibu na kushirikiana na jamii ya wenyeji mkoani hapa." Aliungeza, "Tunavyoendelea kutekeleza Programu ya Pamoja ya Kigoma, tunalenga kujenga mwitikio huu na hatimaye kupanua KJP ili kuzifikia jamii za wenyeji nyingi zaidi mkoani hapa. Kwa kushirikiana na Norway, KOICA na Sweden, UN iko hapa ili kuunga mkono juhudzi za Serikali katika kuhakikisha kuwa hatua za kibinadamu zinazochukuliwa hazizuii maendeleo".

Mwaka jana, Umoja wa Mataifa ulizindua Programu ya Pamoja ya Kigoma (KJP) ili kuunganisha mwitikio wa sasa wa UN kwa mgogoro wa wakimbizi na wahamiaji lakini kwa kuweka mkazo zaidi katika maendeleo ya jamii za wenyeji. Programu ilizinduliwa kwa kushirikiana na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, wanachama wa Kundi la Washirika wa Maendeleo, vyombo vya habari, Vyama vya Kiraia, wakimbizi, wahamiaji na jamii za wenyeji wa mkoa wa Kigoma. KJP inahusisha mashirika 16 ya UN am-bayo yanashirikiana katika maudhui sita



A young woman who benefitted from the UN's previous joint programme in Kigoma Town displays her liquid soap which is one of the products she produces as an entrepreneur. On the far right is UN Resident Coordinator, Mr. Alvaro Rodriguez and to his left is Kigoma District Commissioner, Mr. Samson Anga. Photo| Msafiri Manongi/KJP

## Mafanikio ya Programu ya Pamoja ya Kigoma

### Mafanikio ya Programu ya Pamoja ya Kigoma

Warsha kwa ajili ya wadau wa Programu ya Pamoja ya Kigoma (KJP) iliandaliwa wilayani Kasulu mwishoni mwa Aprili. Ilihudhuriwa na wajumbe wa Baraza la Ushauri la Mkoa (RCC), viongozi waandamizi wa serikali wanaofanya kazi mkoani humo na maofisa wa programu kutoka mashirika 16 ya Umoja wa Mataifa.

Katika hotuba yake ya ufunguzi, Mkuu wa Mkoa, Brigedia Generali (mstaafu) Emmanuel Maganga alitoa shukrani kwa Mratibu Mkazi wa UN, Bw. Alvaro Rodriguez na Timu ya Nchi ya Menejimenti ya UN kwa kuupa mkoa wa Kigoma kipaumbele. Alizishukuru pia serikali za Norway, Korea na Sweden.

Kuhusu upana na maudhui ya programu, Brigedia Generali Maganga alitoa wito kwa Washirika wa Maendeleo kuipanua ili ihusishe wilaya nyingine za mkoani humo pamoja na sekta nyingine. "Hivi sasa programu inashughulikia wilaya za Kibondo, Kakonko na Kasulu, laki ni changamoto za mkoa zimeenea katika wilaya zake zote.

"Kwa kuwa serikali imedhamiria kuleta maendeleo kwa mkoa mzima, tunawaomba washirika wetu kufikiria kuipanua programu hadi kwenye wilaya nyingine na pia kuingiza sekta nyingine—hasa afya, ambayo ina chan-gamto kubwa kwa jamii za wenyeji," alisema.



Mkuu wa Mkoa wa Kigoma Brigedia Generali (mstaafu) Emmanuel Maganga (aliyesimama) akifungua mukutano wa wadau wa KJP. Aliishukuru UN na wahisani wanaowezesha KJP. **Picha| Msafiri Manongi/KJP**



Mratibu wa Eneo la UN la Kigoma, Bw. Evance Siangicha, akiiezwa kwamba KJP inahusisha mashirika 16 ya UN yanayoshirikiana katika maudhui sita (6) ili kuleta maendeleo ya wenyeji mkoani Kigoma. **Picha| Msafiri Manongi/KJP**

Kwa niaba ya UN, Mratibu wa Eneo wa KJP, Bw. Evance Siangicha alizishukuru mamlaka za mkoa na wilaya kwa ushirikiano amba wamekuwa wakitoa tangu kuanza kwa programu hiyo. Aliwahakikisha wadau kwamba UN ilikuwa imedhamiria kuhakikisha kuna kupiga hatua katika kuelekea kwenye Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs). "Mashirika 16 ya UN ni sehemu ya programu hii ya pamoja inayokusudiwa kuchangia katika juhudi za serikali kuimarishe njia za kujipatia riziki za wakazi wa Kigoma. Tunaamini kwamba kwa ushirikiano kati ya wadau wote, lengo hili litafikiwa," alisisitiza Bw. Siangicha.

Kuhusu utekelezaji, wajumbe wa RCC na washiriki wengine walipongeza ushirikiano wa mamlaka za mitaa ambapo kutokana na ushirikiano huo tayari matokeo ya likuwa yameanza kuonekana katika mwaka wa kwanza wa utekelezaji programu.

Waliwaasa maofisa wa programu wa UN kuendelea kushirikiana na maofisa wa mkoa ili kuhakikisha kwamba programu inafanikiwa na kwamba mkoa wa Kigoma unapiga hatua katika kufikia Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs).

*"Mashirika 16 ya UN ni sehemu ya programu hii ya pamoja inayokusudiwa kuchangia katika juhudi za serikali kuimarishe njia za kujipatia riziki za wakazi wa Kigoma. Tunaamini kwamba kwa ushirikiano kati ya wadau wote, lengo hili litafikiwa,"*

**Bw. Siangicha alisisitiza**

## Mafanikio ya Programu ya Pamoja ya Kigoma



Mchambuzi Programu wa UN Women, Bi. Lucy Tesha, akitoa mada iliyoeleza kwamba Tanzania ina viwango vibaya vya ukatili wa jinsia. Alieleza kwamba UN Women ina mpango wa kuendesha kampeni ya elimu kama sehemu ya KJP ili kuwaelimisha watu juu ya athari za vitendo vya ukatili wa kijinsia. **Picha| Msafiri Manongi/KJP**

### UNFPA builds capacity of health workers In Zanzibar

Jumla ya akina mama 310 kati 100,000 hupoteza maisha kila mwa-kaka wakati wa kujifungua huko Zanzibar. Vingi ya vifo hivi husababishwa na kutokwa na damu nyingi, uzazi pingamizi na matokeo ya utoaji mimba kwa njia zisizo salama. Kwa kila mwanamke anayepoteza maisha kwa sababu ya matatizo ya ujauzito, inakadiriwa kuwa kati 20 hadi 30 wengine hupatwa na maradhi sugu au makali. Vingi ya vifo hivi vya akina mama na maradhi vinazuilika endapo kutakuwa na huduma za dharura kukabili uzazi pingamizi, kuwepo kwa mkunga mwenye mafunzo na uzazi wa mpango.

Kufanya hali ya kuwa mama kuwa salama ni haki ya binadamu, na hii ndiyo kiini cha jukumu la Shirika la Umoja wa Mataifa la Idadi ya Watu (UNFPA). Kwa kutambua umuhimu wa kuimariswa Huduma za Dharura katika Uzazi na Matunzo ya Watoto Wachanga (EmONC) huko Zanzibar, UNFPA ilianza kushirikiana na Wizara ya Afya mwishoni mwa mwaka 2016 juu ya programu ya utoaji mafunzo kwa usimamizi ili kutatua upungufu wa maarifa na ujuzi mionganii

mwa watoa huduma za afya. Mada-ktari waandamizi wawili wa masuala ya uzazi na akina mama walipangawa katika vituo vya afya vya Unguja na Pemba ili kuwaongoza madaktari, maofisa afya na wakunga kwa lengo la kuongeza ujuzi na uwezo wao. Dkt. Ramadhan, ambaye amehitimu udaktari wake hivi karibuni, alipangawa kufanya kazi katika kitengo cha uzazi cha Hospitali ya Wilaya ya Wete (Pemba) mnano Mei, 2017. Baada ya kuanza kazi, alijiona kwamba hakuwa na ujasiri wa kutoa baadhi ya matibabu. "Ningalipenda kufanya upasuaji wa kumsaidia mama kujifungua, lakini nakosa ujasiri wa kutosha kufanya hivyo peke yangu," Dkt. Ramadhan alisema wakati huo.

Dkt. Ramadhan alipata msaada wa kufanya mafunzo ya tiba kwa vitendo na baada ya muda, alijengeka zaidi kiustadi kwa kusaidiwa na mtaalamu wa afya mwagine mwenye uzoefu. Hadi kufika Machi, 2018 alikwisha-fanya upasuaji wa kuzalisha akina mama mara 40 bila kuhitaji usimamizi, na ameimarisha uwezo wake wa kutoa huduma za EmONC. Kwa ku-

jenga ujuzi wake na ujasiri, ameokoa maisha.

Alipoulizwa kuhusu tofauti katika programu ya usimamizi katika mafunzo na namna yalivyomsaidia, alisema "Ninajisikia kuwezesha sana katika kuokoa maisha ya akina mama na watoto wachanga hapa Zanzibar. Najikisikia kwamba kuna kitu nafanya, hata kama ni kidogo namna gani, hii inanipa furaha kwenye nafsi na mimi ninajisikia kuwa wa manufaa kwa kuihudumia jamii".



Dkt. Ramadhan ni mmoja wa madaktari waliopata msaada wa mafunzo ya kusimamiwa kwa vitendo; kwa kipindi chote cha kuwa chini ya daktari bingwa aliweza kujenga ujasiri wa kuchukua vitendo mbalimbali. **Picha| UNFPA Zanzibar**

## Ripoti Maalumu: Siku ya Kimataifa ya Wanawake Yaadhimishwa Kimtindo

Katika kuzindua maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Wanawake tarehe 8 Machi, zaidi ya makampuni binafsi 20 yaliyosajiliwa katika Soko la Mitaji la Dar es Salaam (DSE) yaliungana na UN Women na UN Global Compact katika ‘Kugonga Kengele Kuhamasisha juu ya Usawa wa Jinsia’, hii ikiwa ni kwa mara ya kwanza kabisa nchini Tanzania. Hii ni sehemu ya jithada ambayo inashirikisha zaidi ya Masoko ya Mitaji 50 duniani kote, ambapo ‘Kugonga Kengele Kuhamasisha juu ya Usawa wa Jinsia’ inalenga kutoa elimu kuhusu umuhimu wa usawa wa jinsia katika biashara na ajenda ya maendeleo endelevu.

Ikiiongozwa na UN Women Tanzania na Mtandao wa UN Global Compact Tanzania, kampeni hiyo inasisitiza umuhimu wa makampuni kutimiza wajibu wao katika kushajiisha uwezeshaji wanawake kiuchumi na ujumuishi wa kifedha, kuunganisha usawa wa jinsia kama masharti ya kuyafikia Malengo ya Dunia. Vilevile inahamasisha ushiriki kamili na wenye tija wa wanawake, na fursa sawa za uongozi katika ngazi zote za utoaji uamuvi. Makampuni ya sekta binafsi na masoko ya mitaji yanahimizwa kuweka ahadi zenyne kuleta tofauti ili kuendeleza usawa

wa jinsia, licha ya kutumia njia unganishi ya kuibua uwezo wa wanawake katika biashara na jamii.

Akishiriki kama mgeni rasmi, Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Bi. Sihaba Nkinga, alitoa wito kwa makampuni yote binafsi yaliyoorodheshwa katika Soko la Mitaji la Dar es Salaam kuongeza juhudhi katika kushajiisha usawa wa jinsia. Alisisitiza kwamba wajibu wao katika kutengeneza nafasi za ajira, kuwekeza na kuvumbua una nafasi ya pekee katika kuleta uwezeshaji kiuchumi kwa wanawake.

Akizungumza katika tukio hilo, Mratibu Mkazi wa UN, Bw. Alvaro Rodriguez, alisema, “Ikiwa tunataka kuifanya ahadi hii ya Malengo ya Maendeleo Endelevu kuwa kweli, na kutomwacha yeyote nyuma, tunachohitaji kufanya ni juhudhi za haraka kuhusu usawa wa jinsia na uwezeshaji wanawake, na hasa katika sekta binafsi.”

Akigusia juu ya kasi ya upigwaji hatua katika kupunguza tofauti za malipo kati ya jinsia duniani, Mwakilishi wa UN Women, Bi. Hodan Addou, alisema, “Tunajua kwamba ingawa sekta binafsi inatambua kwamba kuleta usawa wa jinsia

katika uendeshaji biashara na minyororo ya thamani kuna maana ya kuleta vipawa zaidi, kuongeza uzalishaji, kuleta wateja zaidi, na kuwa na msingi imara, bado maendeleo ni ya chini. Utatifi wa Jukwaa la Biashara Duniani (WEF) un-aonyesha kwamba, katika kasi ya sasa, itachukua miaka 217 kutatua tofauti za kiuchumi kwa jinsia kote duniani. Hatuwezi kusubiri muda wote huo kuleta mabadiliko hayo: Wakati ni Huu.”

Tukio lililofanyika katika Soko la Mitaji la Dar es Salaam lilifuatiwa na lingine siku ya pili yake katika Soko la Mchikichini, Wilaya ya Ilala ambapo Shirika la Umoja wa Mataifa la UN Women limekuwa likiwasaidia wanawake wafanyabiashara tangu mwaka 2015. Shirika la Kitanza, Equality for Growth (Usawa kwa Maendeleo), likifadhiliwa na UN Trust Fund to End Violence against Women

*“Ikiwa tunataka kuifanya ahadi hii ya Malengo ya Maendeleo Endelevu kuwa kweli, na kutomwacha yeyote nyuma, tunachohitaji kufanya ni juhudhi za haraka kuhusu usawa wa jinsia na uwezeshaji wanawake, na hasa katika sekta binafsi.”*

**Bw. Alvaro Rodriguez, Mratibu Mkazi wa UN**



Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Bi. Sihaba Nkinga (katikati) akigonga ‘Kengele ya Usawa wa Jinsia’ katika Soko la Mitaji la Dar es Salaam katika Siku ya Kimataifa ya Wanawake. Kulia ni Mwakilishi wa UN Women, Bi. Hodan Addou. **Picha| Edgar Kiliba/UNRCO**

**Inaendelea Ukurasa wa 8**



Washirika wa Maendeleo, maofisa wa serikali, maofisa wa UN, wafanya biashara na wadau wengine wakishiriki katika tukio la Kugonga Kengele ya Usawa wa Jinsia katika Soko la Mitaji la Dar es Salaam katika Siku ya Kimataifa ya Wanawake. **Picha| Edgar Kiliba/UNRCO**

## TAARIFA KUHUSU SOKO

Katika mwaka 2016 peke yake, wanasheria waunga mkono jamii waliopata mafunzo chini ya programu waliwasaidia wanawake 454kutoa taarifa juu ya matukio ya ukatili.

(Mfuko wa Udhamini wa UN wa Kumaliza Ukatili dhidi ya Wanawake) unatekeleza mradi unaoitwa, "Toa Malipo, Si Kunyanyasa: Kuwalinda Wanawake Wafanyabiashara Wasio Rasmi wa Dar es Salaam dhidi ya Ukatili kwa Wanawake". Mradi huo umesaidia zaidi ya wanawake 8,000 katika masoko ya mita-

ani kote Dar es Salaam kwa kuwaanzishia maeneo salama ya kufanya biashara ili kuwaondolea ukatili na unyanyasaji. Jambo hili limewaweze-sha kufanya biashara zao kwa uhuru wakitumia haki zao za kiuchumi na kufikia malengo yao ya kiuchumi, ukiachia mbali kuwapa uhuru zaidi wa kifedha na katika kutafuta masoko.



Mwakilishi wa UN Women (OIC), Bi. Hodan Addou, akicheza huku akielekea katika jukwaa tayari kutoa hotuba katika maadhisho ya Siku ya Kimataifa ya wanawake katika soko la Mchikichini. Bi. Addou alitoa pongezi kwa hatua inayopigwa kuelekea katika Usawa wa Jinsia katika soko hilo ambapo sasa kuna uwiano wa 50/50 kati ya wafanyabiashara wa kiume na wa kike. **Picha| Edgar Kiliba/UNRCO**

## Ripoti Maalumu: Siku ya Kimataifa ya Wanawake Yaadhimishwa Kimtindo



Wanawake wafanyabiashara katika Soko la Mchikichini, Ilala, Dar es Salaam, wakisherehekea Siku ya Kimataifa ya Wanawake. UN Women imekuwa ikiwasaidia wanawake wafanyabiashara katika masoko ya mitaani kote jijini Dar es Salaam tangu mwaka 2015. **Picha | Edgar Kiliba/UNRCO**



Mkuu wa Ushirikiano wa Maendeleo katika Ubalozi wa Sweden nchini Tanzania, Bw. Ulf Källstig, akieleza umuhimu wa Usawa wa Jinsia mahali pa kazi. **Picha | Edgar Kiliba/UNRCO**



Watoa burudani wakiendelea na kazi yao katika Siku ya Kimataifa ya Wanawake katika Soko la Mchikichini, Ilala, Dar es Salaam. **Picha | Edgar Kiliba/UNRCO**

## TIMUN 2018: Ushiriki wa Vijana katika Udadisi na Ubunifu kwa Hatima Endelevu



Wajumbe wa Kimataifa na wa Tanzania wakifuatilia sherehe za ufunguzi wa Tanzania International Model UN (TIMUN) 2018 zilizofanyika Dodoma. Picha | Grace Mongi/UNRCO

Modeli ya Umoja wa Mataifa ya Tanzania (Tanzania International Model United Nations (TIMUN)) ni mukano wa kila mwaka wa vijana unaowaleta zaidi ya washiriki 200 kutoka katika nchi wanachama wa Umoja wa Mataifa katika baraza kuu ili kujadiliana kuhusu mada na maudhui yaliyochaguliwa.

TIMUN ya mwaka huu iliwakutanisha washiriki kutoka Tanzania, Uganda, Ghana, Nigeria, Kenya, India, Somalia, Sudani Kusini, UK na Zimbabwe ambao waliketi kwa juma zima waki-jadiliana na kushiriki katika shughuli mbalimbali zinazohusiana na ‘Ushiriki wa Vijana katika Utafiti na Ubunifu’.

Kwa miaka kadhaa, UN Tanzania imekuwa ikifadhili shughuli za TIMUN kifedha na kwa njia ya mafunzo, uwasilishaji na uwezeshaji wa tukio. Ilikuwa ni katika TIMUN 2016 ambapo UN Tanzania ilitoa mafunzo kwa kundi la kwanza la vijana 50 ili wawe Machampioni Vijana wa Malengo ya Dunia na ambao walipewa jukumu la kutangaza Malengo ya Dunia wakilenga kuwafikia vijana 25,000 (ana kwa ana) kila mwaka.

TIMUN 2018 sasa iko mwaka wa pili tangu ushirika huu uanzishwe ambapo zaidi ya vijana 45,000



Naibu Waziri wa Nchi katika Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulika na Sera, Masuala ya Bunge, Ajira, Kazi, Vijana na Walemavu (kushoto) akitembelea maonyesho ya One UN baada ya kufunguliwa kwa TIMUN 2018. Alipokelewa na Ofisa wa Ushirika na Mawasiliano kutoka Ofisi ya Mratibu Mkazi wa UN, Bi. Nafisa Didi. Picha | Grace Mongi/UNRCO

## TIMUN 2018:

### Ushiriki wa Vijana katika Udadisi na Ubunifu kwa Hatima Endelevu

kote nchini wamepewa mafunzo.

Hafla ya TIMUN 2018 ilihudhuriwa na Mh. Antony Mavunde, Naibu Waziri wa Nchi katika Ofisi ya Waziri Mkuu anayesimamia Sera, Masuala ya Bunge, Kazi, Ajira, Vijana na Walemvu.

Akizungumza wakati wa ufunguzi katika ukumbi wa Treasury Square, Mh. Mavunde, alisema, "Tunaamini, mawazo yenu yatachangia juhudii za kutekeleza Ajenda ya 2030.

"Ungaji wenu mkono pamoja na kupaza kwenu sauti kutatoa elimu na hata kupanua wigo wa ufikiwaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu katika jamii zetu."

Akizungumza kabla ya kuanza kwa TIMUN 2018, Mratibu Mkazi wa UN, Bw. Alvaro Rodriguez, alisema kwamba Ajenda ya Maendeleo Endelevu ya 2030 inahitaji ushiriki wa kila mmoja.



Mbunge wa Nzega Mjini, Mh. Hussein Bashe, akiwahutubia vijana wakati wa TIMUN 2018 kuhusu ubunifu na namnagani vijana wanaweza kutumia udadisi kutekeleza Malengo ya Dunia. [Picha | Bunge](#)

"TIMUN 2018 imekuja katika wakati mwafaka...kwa kutazama masuala ya udadisi na ubunifu tunaona njia mpya ya kufasiri SDGs katika hali halisi hasa kwa ajili ya watu maskini na wale walio nyuma," al-

isema Bw. Rodriguez. "Tutaendelea kufanya yote tunayoweza ili kuunga mkono kazi hii muhimu mnayofanya na nina matarajio ya kufanya majadiliano ya mafanikio na changamoto mlizokabiliana nazo," alisema.

Baadhi ya maazimio yaliyowekwa na vijana ni pamoja na:

-Serikali itoe huduma za bure kwa mama na mtoto ili kupunguza idadi ya vifo akina mama

-Majukwaa yenyewe gharama nafuu ya kutoa mafunzo kwa vijana yaanzishwe ili kuwapa uhakika wa kupata kazi katika taasisi za umma na binafsi

-Wito kwa wanachama wote ili kuhakikisha usawa katika uwezeshejji katika kupata rasilimali na mali zote kwa kulinaganisha na usawa wa kijinsia.



Machampioni Vijana wa Malengo ya Dunia ambao wamekuwa wakiendesha shughuli za kueneza elimu juu ya utekelezaji wa Malengo ya Dunia nchini Tanzania tangu TIMUN 2016. [Picha | Didi Nafisa/UNRCO](#)

## TIMUN 2018: Ushiriki wa Vijana katika Udadisi na Ubunifu kwa Hatima Endelevu



Championi wa Malengo ya Dunia, Bw. Lameck Lawrence, akitoa mafunzo juu ya Malengo ya Dunia wakati wa shughuli ya TIMUN 2018. **Picha | Grace Mongi/UNRCO**



Naibu Waziri wa Nchi katika Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mh. Joseph Kakunda, akipokea maazimio ya TIMUN 2018 kwa niaba ya Serikali. Kabla hajafunga kongamano, aliwahamasisha vijana kutekeleza Malengo ya Dunia. **Picha | Grace Mongi/UNRCO**



Washiriki wa TIMUN 2018 wakihudhuria moja ya vipindi vya Bunge. Walialikwa na Naibu Waziri wa Nchi katika Ofisi ya Waziri Mkuu, Mh. Anthony Mavunde. **Picha | Bunge**

## UNICEF Hands Over Newly Constructed Mugeza Mseto Primary School

Hivi karibuni, UNICEF Tanzania ilik-abidhi kituo kipywa kilichoengwa cha Shule ya Msingi ya Mugeza Mseto ya Buko kwa ajili ya Wenye Mahitaji Maalumu ba ambayo iliathiriwa na tetemeko la ardhi la Septemba, 2016.

Shule hiyo iliyofanyiwa marekebisho, hivi sasa ina madarasa matatu, mabweni manne ya watoto 192 wenyewe ulemavu; vyumba viwili vya kujitakasa – kimoja kwa wavulana na kingine kwa wasichana—ambavyo vyote vimeundwa kuwezesha matumizi ya watoto wenyewe ulemavu; na pia kuna chumba cha wagonjwa kikiwa na vifaa vyote kwa ajili ya matumizi ya kulazwa hata usiku.

Kufuatia tetemeko baya lililoukumba Mkoa wa Kagera, UNICEF iliomba na Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof Joyce Ndalichako, kusaidia kuikarabati shule hiyo ili watoto walioathiriwa wapate nafasi ya kuendelea na safari yao ya kujifunza. Tetemeko la ardhi liliharibu kabisa majengo 840 ambapo zaidi ya nyumba 1,200 zilipata uharibifu mkubwa na kuwafanya maelfu ya watu kukosa makazi, huku wanafunzi, wakiemo wa Shule ya Msingi ya Mugeza Mseto ya Watoto wenyewe Mahitaji Maalumu, kukosa madarasa, vyoo,



Watoto wawili wakitabasamu kwa furaha wakati wa moja ya ziara za kusaidia watoto walio hatarini. **Picha |MAKTABA**

mabweni na nyumba za walimu. Majengo yataimarisha utoaji wa upatikanaji wa elimu bora, yenyewe usawa na jumuishi kwa watoto 763, mionganii mwao 397 ni wasichana. Katika wanufaikaji, 150 ni watoto wenyewe ulemavu wakiwemo wasichana 68. Licha ya hilo, shule hiyo sasa ina huduma bora kwa ajili ya WASH (maji, usafi wa mazingira na wa mwili)," alisema Maniza Zaman katika hotuba yake ya kukabidhi ambayo

ilitolewa kwa niaba yake na Mtaalamu wa Elimu wa UNICEF, Bi. Cecilia Baldeh.

Kaimu Mkurugenzi wa Manispaa, Bw. Lukiko, aliishukuru UNICEF na Klabu ya Rotary kwa msaada wao na alipongeza jamii zinazoizunguka shule kwa ushirikiano na michango yao iliyowezesha ukarabati wa shule kufanikiwa.



Moja ya darasa lililokarabatiwa na UNICEF baada ya tetekemo la ardhi la Septemba, 2016 mkoani Kagera. **Picha |UNICEF Tanzania**

## Mkurugenzi wa Kanda wa WFP na Mkuu wa Mkoa wa Dodoma wafanya ziara katika maeneo ya miradi

Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Dkt. Binilith Mahenge, na Mkurugenzi wa Kanda ya Kusini mwa Afrika na Nchi za Bahari ya Hindi wa Shirika la Mpango wa Chakula Duniani, Bi. Lola Castro, wakitembelea shughuli za WFP katika Ofisi Ndogo za Dodoma mwezi Machi na Aprili. Bi. Castro alitembelea maeneo ya mradi wa lishe na kilimo unaofadhiliwa na WFP na kukutana na washirika na maofisa mbalimbali wa serikali mkoani Dodoma. Wakati wa ziara yake katika Kikundi cha Wakulima cha Chawanako chini ya Mpango wa Ushirika wa Tangu Shambani Hadi Sokoni (Farm to Market Alliance (FtMA)) wilayani Kibaigwa, Bi. Castro alieleza kwamba WFP imekuwa ikifanya kazi nzuri nchini Tanzania na kwamba wakulima walikuwa an shauku ya kupata taarifa, mafunzo na ujenzi wa uwezo zaidi kuhusu taratibu za kilimo bora, upatikanaji wa pembejeo bora, masoko yanayotabirika na kupunguza hasara ya baada ya mavuno.

Bi. Castro pia alitembelea miradi ya Jamii za Kupunguza Kabisa Njaa za Saemaul (Saemaul Zero Hunger Community projects (SZHC)) katika Kijiji cha Suli. Miradi hiyo inafadhiliwa na Shirika la Kimataifa la Ushirikiano la Korea (KOICA), WFP na Good Neighbours International (GNI). Alikutana na wanufaikaji wa mradi wa mbuzi, kuku, ufugaji nguruwe na umwagiliaji.

Tangu 2014, SZHC zimewanufaisha zaidi ya watu 12,280 katika vijiji vitatu (Fufu, Suli na Chiboli) katika Wilaya ya Chamwino. Ujenzi wa miradi ya umwagiliaji ulianza mwa-kaka 2017 kama sehemu ya mradi wa mashamba ya ufta. Mradi unawalenga vijana, wanawake na watu walio hatarini zaidi 100 na ni mionganini mwa miradi ya jamii saba inayolima na kuza ufuta kuitia programu hiyo.



Bw. Saleh Abdullah (kushoto) na Bi. Lola Castro (katikati) wakitembelea kikundi cha wakulima wadogo chini mpango wa FtMA huko Kibaigwa. [Picha | Pendo Nkya/WFP](#)

Kabla ya zaira ya Bi. Castro, Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Dkt. Binilith Mahenge, alitembelea vijiji vitatu cha SZHC ili kukagua miradi ya umwagiliaji na kujionea changamoto wanazokabiliana nazo wanavijiji katika maisha yao ya kila siku. Dkt. Mahenge alishukuru KOICA, WFP na GNI kwa ufadhili, akiongezea kwamba vijiji hivyo vilikuwa na bahati ya kuchaguliwa kati ya vijiji 32 vya Chamwino. Alisisitiza kuhusu ushiriki motomoto na umiliki wa miradi.



Dkt. Binilith Mahenge, Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, akitembelea eneo la mradi wa umwagiliaji huko Chiboli. [Picha | Serena Okawa/WFP](#)

## UN, Serikali kuimarisha ushirikiano katika kutoa taarifa na kufanya utetezi wa pamoja

Umoja wa Mataifa umeeleza nia yake ya kushirikiana na Chama cha Maofisa wa Mawasiliano wa Serikali Tanzania (TAGCO) katika jithi-hada za kuimarisha mawasiliano ya pamoja yanayohusisha serikali na UN. Pande hizo zimetengenza ushirika ambao utaratibu kwa karibu uratibu wa amali mahsusizi za serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Umoja wa Mataifa.

Ushirika unaokusudiwa unalenga kuimarisha utoaji taarifa za maendeleo yaliyokwishapati kana katika utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano (FYDP II), Mpango wa Pili wa Msaada wa Maendeleo wa Umoja wa Mataifa (UNDAP II) na Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs).

Akizungumza katika mukutano wa ujenzi wa uwezo wa TACGO katika Ukumbi wa Kimataifa wa Mikutano wa Arusha (AICC), Mratibu Mkazi wa UN, Bw. Alvaro Rodriguez, alisema "Tungependa kushirikiana kwa karibu na maofisa mawasiliano wa serikali ili kutoa taarifa kuhusu utekelezaji wa SDGs kama yanavyope-



Maofisa mawasiliano wa serikali wakifuatilia uwasilishaji kuhusu Malengo ya Dunia uliofanywa na Mratibu Mkazi wa UN, Bw. Alvaro Rodriguez. **Picha | Edgar Kiliba/UNRCO**

wa kipaumbele katika Mpango wa Pili wa Maendeleo ya Taifa (FYDP II) na MKUZA III. Naamini kupitia ushirika huu, tunaweza kuhakikisha Tanzania tunayoitaka inafikiwa kupitia utan-gazaji kazi za serikali na michango ya UN katika maendeleo ya Tanzania".

Mratibu Mkazi wa UN alitoa wito kwa pande mbili hizi ushirikiana katika utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs). Alisitisiza kwamba maeneo ya ushirikiano kati ya UN na serikali yata-jumuisha mawasiliano ya pamoja kuhusu maadhimisho na ziara; ute-tezi wa pamoja na utayarishaji wa mkakati wa mawasiliano ya SDGs.



Msemaji Mkuu wa Serikali, Dkt. Hassan Abbas akieleza kuwa Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo inafanyia kazi kanuni za ushirikiano na UN ambazo zitahusisha utetezi wa pamoja na utoaji taarifa za wpamoja katika kutekeleza Mpango wa Pili wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano na Malengo ya Dunia. **Picha | Edgar Kiliba/UNRCO**

Ushirika huu unakusudiwa kuongeza ushirikiano kati ya Kikosi cha Mawasiliano cha UN (UNC), ambalo ni kundi muhimu la mawasiliano kwa mashirika yote ya UN yenye ofisi nchini Tanzania, na maofisa wa mawasiliano wa serikali.

Kwa upande wake, Msemaji Mkuu wa Serikali, Dkt. Hassan Abbas, alieleza kwamba Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo ilikuwa ikifanya kazi makubaliano rasmi juu ya utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano na Malengo ya Dunia. Alisema kwamba, mafunzo yataangazia maeneo kama vile kupeleka vyombo vya habari katika ziara na kuona mchango wa miradi iliyofanikiwa..

## Umahiri wa kuandika habari za watoto: Jukwaa lwa Wahariri Tanzania & UNICEF zawatunuku waandishi wa habari

Mwishoni mwa Aprili, waandishi wa habari 11 wa magazeti na dijitali walitambuliwa kwa umahiri wao wa kuandika habari zinazohusu masuala ya watoto, hii ikiwa ni mara ya kwanza kabisu kwa Tuzo kwa Waandishi wa Habari iliyoandaliwa na Jukwaa la Wahariri Tanzania (TEF) kwa msaada wa kiufundi wa UNICEF. Tuzo hiyo ilitokana na ushirika kati ya TEF na UNICEF, ambazo kwa pamoja zilianzisha Kundi la Wahariri Machampioni kwa ajili ya Haki za Watoto (ECGCR). Sherehe za tuzo zilifanyika Morogoro ambapo Mwakilishi wa UNICEF Tanzania, Bi. Maniza Zamani, alikuwa mgeni rami na aliwaponeza TEF na waandishi kwa kujitoa kwao na mapenzi yao katika kuleta ushirika wenye tija. Washindi wa tuzo walikuwa miongoni mwa waandishi 40 waliopata mafunzo kupitia ushirikiano huu. Bi. Tumaini Msowoya wa Kampuni ya Mwananchi Communications Limited aliibuka mshindi wa jumla na alipokea Tuzo ya Utendaji Bora Kuliko Zote si tu kwa kuchapisha zaidi ya habari 25 kuhusu masuala ya watoto bali pia habari zake zilikuwa bora zikieleza kwa



Bi. Tumaini Msowoya, mwandishi kutoka Gazeti la Mwananchi na Kitengo cha MCL Dijitali, aliyekuwa mshindi wa jumla akishangilia kwa tuzo yake aliokabidhiwa na Mwakilishi wa UNICEF, Bi. Maniza Zaman. **Picha | UNICEFTZ**

ufasaha masuala ya watoto. "Habari zetu ni njia ya kusamba za welewa kwa umma na kupaza sauti za wale walio wanyonge kabisa na kuzifikisha kwa wenye jukumu la kuzitatua. Watoto wanafanya takribani nusu ya idadi ya watu Tanzania, na hivi sasa wanakabiliwa na changamoto nyinigi. Kutambuliwa kwa juhudini zangu kuna maana kubwa sana kwangu

hasa katika kutangaza zaidi masuala yanayowasibu watoto nchini. Najisikia furaha sana na ninatumia fursa hii kuzungumza kwa niaba ya washindi wote leo kwamba tuko tayari kuendelea kutetea masuala ya watoto, na tutaendelea kuchunguza yale yanayokwamisha maendeleo ya watoto Tanzania," alisema Bi. Msowoya. "Tuzo hii ni ishara kwa mafanikio makubwa ya ECGCR. UNICEF inafuraha kushirikiana na kundi hili na kutoa msaada wa kiufundi. Kikosi kazi cha waandishi 40 waliopata mafunzo kama sehemu ya ushirikano huu wamekuwa machampioni wa masuala ya watoto nchini na wamesaidia kuleta msukumo. Ninawapongenza washindi kwa kuandika habari makini kuhusu masuala ya watoto," alisema Bi. Zaman. "wa upande wake, Kaimu Mwenyekiti wa TEF, Bw. Deodatus Balile, alisema ushirika na UNICEF umekuwa na mafanikio makubwa na umesaidia wahariri na waandishi wa habari kuibua masuala mengi yanayowakabili watoto nchini Tanzania.



Waandishi wa habari 11 walioshinda tuzo za umahiri katika kuandika juu ya masuala ya watoto wakiwa pamoja na Mwakilishi wa UNICEF, Bi. Maniza Zaman, na Kaimu Mwenyekiti wa TEF, Bw. Deodatus Balile. **Picha | UNICEFTZ**

## UNCDF na serikali zajenga Kituo Kikuu cha Mabasi cha Kibaha



Kituo Kikuu kipywa cha mabasi cha Halmashauri ya Mji wa Kibaha kikiwa katika hatua za mwisho za ujenzi. Picha | UNCDF

Halmashauri ya Mji wa Kibaha (KTC) inajenga kituo kikuu cha mabasi cha kisasa chenye uwezo wa kupokea takribani mabasi 600, mabasi madogo 1,500 na hadi watu 96,000 kwa siku. Kituo hiki kikuu kipywa ni suluhisho kwa kilio cha watu wa Kibaha kwa huduma hiyo kufuatia kuvunjwa kwa kile cha awali kilichokuwa Maili Moja katika mpango wa kupanua barabara kuu ya Dar es Salaam hadi Chalinze. Mwanzoni, KTC ilitumia fedha ku-

toka vyanzo vyake na pia kutumia fedha zenyne masharti maalumu kutoka serikalini chini ya programu ya Kusaidia Serikali za Mitaa za Miji-ni (ULGSP). Shirika la Umoja wa Mataifa la Mtaji wa Maendeleo (UNCDF) lilitoa msaada wa kiufundi na mtaji wa kuanzia ili kuwesheha mradi huu kuwekezeka. Akizungumza kutoka eneo la mradi, Ofisa Mawasiliano wa KTC, Bw. Innocent Byarugaba, alisema "Mradi utagharimu

takribani Dola za Marekani milioni 1.7 hadi kukamilika na utaongeza vyanzo muhimu vya mapato vya KTC kwa ajili ya kutoa huduma bora zaidi za jamii kwa watu wa Kibaha." Kituo hicho kikuu kitatoa huduma kama kituo cha muda kwa magari yanayotoka na kulekea pande mbalimbali za Tanzania na nchi jirani za Kenya, Uganda, Malawi na Zambia. Inatarajiwa kwamba watu 40,000 watakuwa wakipita katika mji wa Kibaha kila siku. Mradi huo unatumia nguvu kazi ya watu wa Kibaha katika ujenzi na kitakapokamilika, kitatengeneza ajira nyingi katika uendeshaji na matunzo yake. Kinatarajiwa kuongeza kipato zaidi kwa kaya na kuchangia kupunguza umaskini katika maeneo hayo kwa sababu kitaongeza fursa za kiuchumi. Zaidi ya hayo, wafanyabiashara na wajasiriamali wanawake watanufaika kutokana na ongezeko la wasafiri wanaoingia na kutoka katika mji huo. Miundombinu ya nyongeza na huduma nyingine kama vile mitando ya barabara, maji, migahawa, huduma za kibenki na umeme zitaanzishwa ili kuhudumia kituo hicho kikuu.

## Wabunge kutoka Sweden watembelea Zanzibar

Hivi karibuni, Ofisi Ndogo ya UN ya Zanzibar ilipokea ujumbe wa Wabunge watatu kutoka Sweden. Madhumuni ya ziara ya ujumbe huo yalikuwa kujionea wenyewe namna gani UN inasaidia serikali na watu wa Zanzibar katika kutekeleza Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs). Miiongoni mwa miradi mingine, ujumbe ulitembelea Kikundi cha Wanawake cha Furahia cha Biashara ya Mwani katika Kijiji cha Paje, Wilaya ya Kusini Unguja. Katika kijiji hicho, wabunge walipata fursa ya kuzungumza na wanawake hawa wakulima wa mwani na kuona bidhaa zao mbalimbali. Wanawake huwa hushughulika na kilimo cha mwani na uchakataji wake.

Tangu Novemba 2017, Shirika la Umoja wa Mataifa la Chakula na Kilimo (FAO) limekuwa likiwasaidia wanakikundi hawa kumalizia ujenzi wa majengo na kupata mashine za kuchakata mwani na kutengeneza sabuni.

Msaada huo pia unajumuisha mafunzo juu ya namna ya kutumia mashine katika mchakato wa uzalishaji. Kikundi kilianzishwa mwaka 1998 na kuwa mwanachama wa Mradi wa Klasta ya Mwanzi Zanzibar mwaka 2008. Wanachama wake wote wanajishughulisha na kilimo cha mwani na kuongeza thamani kwa kutengeneza bidhaa kama vile sabuni, mafuta ya mwili, keki na huisi.



Wabunge kutoka Sweden wakionja chakula kilichotayarishwa na wanawake wajasiriamali. Picha | UNCDF

## Wabunge kutoka Sweden watembelea Zanzibar



Wabunge kutoka Sweden wakikutana na wanawake wanaolima mwani ambapo walijifunza namna ya kuvuna mwani.



### Siku za Umoja wa Mataifa:

**5 Juni – Siku ya Mazingira Duniani**

**8 Juni – Siku ya Bahari Duniani**

**16 Juni – Siku ya Mtoto wa Afrika**

**26 Juni – Siku ya Mkataba wa Umoja wa Mataifa**

### ***Umoja wa Mataifa Madhubuti kwa Dunia Bora Zaidi !***

**Mabadiliko ya UN kwa ufupi**  
Tanzania ni moja kati ya nchi zin-  
azongoza katika mpango wa  
kufanya kazi pamoja. Tangu Julai  
2016, timu ya wakuu wa Mashiri-  
ka ya Umoja wa Mataifa Tanzania  
wamekuwa wakiufanyia kazi mpan-  
go. Mpango wa Umoja wa Mataifa  
wa kusaidia Tanzania (UNDAP II).  
Kwa taarifa zaidi kuhusu mipango  
na mapitio ya UN tembelea:

[www.undg.org](http://www.undg.org)



### **UN Resident Coordinator's Office**

#### **Communications Specialist**

[hoyce.temu@one.un.org](mailto:hoyce.temu@one.un.org)

Phone : (+255) 22-219-5021



Kwa taarifa zaidi tembelea: [tz.one.un.org](http://tz.one.un.org)